*Kikundi cha sanduku la barua kinawaletea...*



# KIKUNDI CHA WAPELELEZI

Jina

______________________________



WAPELELEZI 1

swa_EC1Workbook_201500309.indd 1 5/7/15 1:12 PM

# MEZA YA YALIYOMO

## MASOMO

1 Je Mungu Yukoje? (Sehemu Ya 1)..............................Ukurasa 1

2 Je Mungu Yukoje? (Sehemu Ya 2)............................Ukurasa 9

3 Sisi Tumetoka Wapi? ..................................................Ukurasa 17

4 Ni nani Adui Yetu?.....................................................Ukurasa 25

5 Ni nani Mwokozi Aliyeahidiwa? .............................Ukurasa 33

6 Yesu, Yu Hai Leo!.........................................................Ukurasa 41

7 Maswali Manne ...........................................................Ukurasa 49

8 Naweza kuwa Mtoto wa Mungu!...........................Ukurasa 57

9 Yesu Anakuja Tena! ....................................................Ukurasa 65

10 Vitu 4 Mungu Anataka Mimi Nijue........................Ukurasa 73

11 Mtu Mpya Katika Kristo............................................Ukurasa 81

12 Zawadi ya Mungu Kubwa Kuliko Zote..................Ukurasa 89

**WAPELELEZI 1 KITABU CHA:** ISBN 978-1-938041-63-1 www.mailboxclub.org

*Haki ya nakala © 2015. Masomo kwa njia ya Posta Kimataifa.*

*Maandiko yamechukuliwa kutoka katika toleo jipya la King James ® Haki ya nakala © na Thomas Nelson, Inc. Imetumiwa kwa ruhusa. Haki zote zimehifadhiwa.*

SOMO LA 1

# JE MUNGU YUKOJE?
## (SEHEMU YA 1)

**Mpendwa Rafiki,**

Je, umewahi kufikiri Mungu yukoje? Mungu ni mkubwa sana na ni wa ajabu sana kiasi kwamba hatuwezi kuelewa kila kitu kuhusu Yeye. Lakini Mungu anatupa kitabu cha ajabu ambacho kinatueleza kuhusu Yeye.

**Je, hiki ni kitabu gani?** Ni Biblia. Neno la Mungu. Biblia inatueleza kwamba Mungu aliumba vitu vyote. Mungu aliumba jua na mwezi. Aliumba mamilioni ya nyota ambazo zinang'aa usiku katika anga juu yetu. Mungu aliumba nchi. Mungu aliumba ndege, samaki, na wanyama. Kisha Mungu aliumba mwanamume na mwanamke wa kwanza.



**Ni kwa nini Mungu alituumba?** Tuliumbwa tumpende Mungu na tupendwe na Yeye. Mungu anamfahamu na anampenda kila mmojawetu.

**Inampendeza Mungu sana** wakati tunapotaka kumfahamu Yeye na kumpenda. Kumfahamu Mungu na kumpenda ni kitu bora sana tunachoweza kufanya.

**Katika Somo hili** tutaona ni nini Biblia inatueleza kuhusu Mungu. Tutajifunza mambo matano muhimu kuhusu Mungu wetuwa ajabuambaye anatupenda sana.



swa_EC1Workbook_201500309.indd 1 5/7/15 1:12 PM

## MUNGU NI NAFSI HAI.

**Kuna Mungu mmoja tu** Mungu wa kweli na anayeishi. Alisema, “Mimi ni Bwana, na hakuna mwingine; Hapana Mungu zaidi Yangu” (Isaya 45:5).

Mungu sio “nguvu fulani”. Mungu ni nafsi hai ambaye anamfahamu na kumpenda kila mmoja wetu. Mungu anapendezwa tunapotaka kumfahamu Yeye. Zaidi ya yote Mungu anataka sisi tumpende kwa mioyo yetu yote.

## MUNGU NI ROHO.

Ingawa Mungu ni nafsi hai, Hana mwili kama tulio nao sisi. Mungu ni ROHO. Hatuwezi kuona kile ambacho ni Roho.Wakati Mungu alipokuumba wewe Alikupa akili. Alikupa pia wewe Roho. Roho yako inaishi ndani ya mwili wako. Watu wengine wanaweza kuuona mwili wako lakini hawawezi kuona Roho yako.

**Mungu ni Roho tupu.** Ndiyo maana hatuwezi kumwona Yeye. Mungu anatuambia tusitengeneze sanamu zozote kumwakilisha Yeye. Mungu anatuambia tusiabudu sanamu yoyote. Biblia inasema, “Mungu ni Roho: nao wanaomwabudu Yeye lazima wamwabudu katika Roho na kweli” (Yohana 4:24).


Ingawa hatuwezi kumwona Yeye, Mungu ndiye wa kweli na anayeishi. Anataka sisi tumjue Yeye. Tukimjua Mungu tutampenda Yeye. Natukimpenda Yeye tutataka kumtii Yeye.

## MUNGU NI WA UTUKUFU.

**Utukufu wa Mungu unangáa** sana kiasi kwamba hatuwezi kumtazama Yeye. Hatuwezi kulitazama jua kwa muda mrefu wakati linapong’aa sana. Linaumiza macho yetu. Kama tungelitazama kwa muda mrefu, tungepoteza uwezo wetu wa kuona.

Utukufu wa Mungu unang’aa kuliko jua. Ndiyo maana hatuwezi kumtazama Yeye. Mungu alisema, “Hakuna mtu atakayeniona Mimi akaishi” (Kutoka 33:20).

**Biblia inatueleza juu va mtu aliyeitwa Musa.** Musa alikuwa rafikimaalumu wa Mungu. Aliongea na Mungu na Mungu aliongea naye mara nyingi. Lakini Musa hakuwahi kumwona Mungu.



Siku moja Musa aliomba upendeleo maalumu kwa Mungu. Alisema, “Tafadhali nionyeshe utukufu wako” (Kutoka 33:18).

**Mungu alimwambia Musa,** “Huwezi kuona uso wangu kwa sababu hakuna awezaye kuniona akaishi. Lakini nitakuficha ndani ya miamba, kisha nitapita pembeni yako”.

**Musa alipanda juu** mlimani peke yake. Mungu alimficha katikati ya miamba. Kisha Mungu alisababisha utukufu wake upite kando ya Musa. Musa hakumwona Mungu, bali aliona sehemu kidogo ya utukufu wa Mungu, na ulisababisha uso wake kung’aa sana.

**Musa aliposhuka chini** kutoka mlimani, uso wake uling’aa sana kiasi kwamba watu walimwogopa. Ndio maana haishangazi kwamba Musa na watu walisema “Ni nani aliye kama wewe, ee Bwana. Mtukufu katika utukufu?” (Kutoka15:11).

## MUNGU NI MTAKATIFU.


**Hii ina maana kwamba Mungu ni msafi na mkamilifu** na pasipo dhambi yoyote kabisa. Katika Biblia, wakati mwingine gizahusimamama badala ya dhambi. Bibliainasema, “Mungu ni nuru, na ndani yakehakuna giza (hakuna dhambi) kabisa” (1 Yohana 1:5).

**Mungu ni nuru yote na utukufu Mungu ni msafi.** Mungu hatendi dhambi. Mungu siku zote amefanya yaliyo mazuri na sahihi. Hakuna chochote chenye dhambi kitakacho kaa katika uwepo wa Mungu. Biblia inasema, “Bwana Mungu wetu nimtakatifu” (Zaburi 99:9).

Mungu aliwahi kuzungumza katika maono na nabii aliyeitwa Isaya. Maono ni kamandoto. Isaya aliona maono ya Mungu katika kiti chake cha enzi. Walikuwepo malaika wengi waliokuwa wamekizunguka kiki Chake cha enzi wakisifu na kusema, “Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu ni Bwana wa majeshi; Nchi yote imejaa utukufu Wake” (Isaya 6:3).

**Isaya alipoona maono hayo ya** Mungu, aliogopa. Maono yalimwonyesha kuwa alikuwa mwenye dhambi na Mungu ni mtakatifu.






## MUNGU NI PENDO.

Hii inamaanisha kwamba Mungu anatupenda si si na anataka kila kilicho bora kwa ajili yetu.

**Twawezaje kujua kuwa Mungu** anatupenda sisi? Twajua njia mbili:

- **Mungu alisema hivyo?** Katika neno lake Mungu anasema, “Ninakupenda kwa upendowamilel” (Yeremia 31:3).
- **Mungu alimtoa mwanawe** kuchukua adhabuya dham bizetu.

**Mungu alionyesha upendo wake mkuu** kwetu kwa kumtoa mwanawe, Bwana Yesu, kufa msalabani kwa ajili ya dhambi zetu mambo mabaya ambayo tunasema na kutenda. Biblia inasema, “Mungu alionyesha pendo lake kwetu tulipokuwa tungali wenye dhambi, Yesu alikufa kwa ajili yetu” (Warumi 5:8).

Waweza kuwa na unafikiri, “Je, Mungu anafahamu mambo yote mabaya ambayo nim esem a na kutenda?” Ndiyo, Mungu anafaham uhayoyote, lakinibado. anakupenda wewe kwa moyo wake wote. Anakupenda wewe kila dakika ya maisha yako.

**Bwana Yesu alikufa kwa dhambi zangu.** Alikufa kwa dhambi zako. Lakini hakubaki mfu. Alifufuka kutoka kaburini siku ya tatu. Ni mwokozi wetu anayeishi! Mungu anataka umwamini Yeye kama aliyekufa kwa dhambi zako na kufufuka tena kuwa mwokozi wako. Je, wajua Mungu anataka ufanye nini zaidi ya yote? Anataka umpende kwa moyo wako wote.

**Inampendeza Mungu** unapochagua kumpenda Yeye kwa moyo wako wote. Mfalme Daudi alikuwa mtu mkuu wa Mungu katika Biblia. Alisema, “Nitakupenda ee Bwana”. Hili lilimpendeza Mungu, na itampendeza Mungu sana kama utachagua kumpenda Mungu kama mfalme Daudi alivyofanya. Hapa kuna sala ya kukusaidia:

**“Mpendwa Mungu, ninafurahi sana kwamba unataka nikupende wewe. Ninataka kukupenda wewe kwa moyo wangu wote. Asante kwa kumpenda hata ukamtoa mwanao, Bwana Yesu, kufa msalabani kwa ajiliya dhambi zangu”.**



swa_EC1Workbook_201500309.indd 4 5/7/15 1:12 PM




## "JE, NAWEZAJE KUWA MTOTO WA MUNGU?"


**A** – *Kubali kwamba wewe ni mwenye dhambi.*

**B** – *Mwamini Bwana Yesu aliyekufa kwa ajili ya dhambi zako.*

**C** – *Njoo kwa Bwana Yesu na umpokee Yeye kama Mwokozi wako.*

*"Bwana Yesu, hakika nasikitika kwa ajili ya dhambi zangu. Naamini kwamba wewe ni mwana wa Mungu na ulikufa kwa ajili ya dhambi zangu. Sasa hivi nakupenda wewe kama Mwokozi wangu".*

# MSTARI WANGU WA MOYO








swa_EC1Workbook_201500309.indd 5 5/7/15 1:12 PM

# KUTAFUTA HAZINA

***Tumia alama za siri zilizopo hapo chini kufumbua fumbo la kuwinda hazina.***








swa_EC1Workbook_201500309.indd 6 5/7/15 1:12 PM

# UKURASA WA MASWALI

## WAPELELEZI 1 SOMO LA 1

**MAELEZO: Chagua jibu sahihi a au b. Andika katika boksi ulilopewa.**

**Mfano: Mbingunini mah aliam bapo kuna**

[ b ] a. dhambi ndogo.
b. hakuna dhambi.

**1. Mungu yukoje?**

[ ] a. Munguni "nguvufulani".
b. Mungu ni nafsi hai inayoishi ambaye anatufahamu na anafup endasisi.

**2. Hatuwezi kumwona Mungu kwa sababu**

[ ] a. Mungu ni Roho na hatuwezi kuona Roho.
b. Mungu yuko mbali sana kiasi kwamba hatuwezi kum wona.

**3. Wakati Biblia in aposem a kwamba Mungu ni mtakatifu, in a maana kwamba**

[ ] a. Mungu ni mzuri sana.
b. Mungu ni msafi na mkamil ifu pasipo dhambi yoyote.

**4. Nafahamu kwamba Mungu ananipenda kwa sababu**

[ ] a. Alimtoa mwanawe afe kwa ajili ya dhambi zangu.
b. Najisikia kama vile anani penda.

**5. Nikitu gani Mungu anataka mimi nifanye zaidi ya yote?**

[ ] a. Mungu anataka nimp end ekwa moyo wangu wote.
b. Mungu anataka nimfanyie mambo mengimazuri.

Andika mstari wa
Moyo wa somo hili hapa:



Andika jibu la fumbo
La kutafuta Hazina:

Jina______________________________ Tarehe ya kuzaliwa___/___/___ Umri ___ Darsa ______
(ANDIKA KWA HERUFI KUBWA) (MWEZI/SIKU/MWAKA) (KAMA NI MTU MZIMA)

Mzazi/Mlezi ________________________________________

Anwani ________________________________________

Mji ____________________ Jimbo _______ Zip ____________________



swa_EC1Workbook_201500309.indd 7 5/7/15 1:12 PM

# SAFARI YANGU NA YESU

1 Nikitu gani muhimuz aidi ulichoj ifunz a kutoka katika somo hili?

2 Je, kuna kitu chochote ambacho hukielewi kutoka katika somo hili?

3 Je, una mahitaji yoyote maalumu au mambo ya kuombea?

4 Tunakutia moyo uanze diary. Andika maombi yako, sifa na shukrani kwa Mungu!



swa_EC1Workbook_201500309.indd 8 5/7/15 1:12 PM

the Mailbox Club

www.mailboxclub.org